# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

**MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA .................**

# SHULE YA SEKONDARI YA LUPEMBE

S.L.P 114 NJOMBE Barua pepe: lupembesekondari@njombedc.go.tz simu/contact
Mkuu wa shule 0768830617, Makamu 0763685895, Mhasibu 0753760283, Mtaaluma 0754231771

**Kumb.Na**. LSS/10/2026

Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi.....................................................
S.L.P..........................
...................................

**YAH: MAAGIZO KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LUPEMBE KIDATO CHA TANO MWAKA .................................**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule ya Sekondari ya Lupembe mwaka huu.

Shule ya Sekondari LUPEMBE ipo umbali wa Kilometa 70 Mashariki mwa Mji wa NJOMBE Usafiri wa basi ni **TSHS 10,000/=** kutoka stendi kuu Njombe mjini hadi shule ilipo.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **.........................,** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti kwa muda mwafaka.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.**

**1. SARE ZA SHULE**

(i) Suruali mbili rangi ya kijivu mpauko suruali mbili (2) bluu bahari zenye mifuko miwili mbele na mmoja nyuma,upana miguu inchi 16 yenye turn up pamoja na mkanda mweusi wa ngozi wa kimasai. T-shirt (form six) itapatikana shuleni kwa bei ya Tsh. 15,000/= tu.

(ii) Sweta mbili rangi ya kijani jeshi Track suit kwa ajili ya maandalizi ya masomo ya jioni na usiku, Mashati meupemawili ya mikono mirefu pamoja na tai ndefu rangi nyeusi na bluu bahari.

(iii) Viatu vya ngozi vyeusi jozi **mbili (2)** vya kufunga na kamba visivyona visigino virefu.

(iv) Pullneck nyeusi moja, Singilent nyeupe **nne (4)** na boxer **tano (5),** koti jeusi lisilo na Kofia wala maandishi kwa matumizi ya nyakati za baridi.

(v) Raba nyeusi za jogging, njumu za uwanjani, jezi rangi ya blue (kaptula na tshirt) isiyo na maandishi na track suit rangi nyekundu yenye mistari myeupe pembeni kwa ajili ya michezo(muhimu sana) Soksi jozi nne (4) au zaidi rangi nyeusi na soksi bluu ndefu za michezo pair mbili (2).

(vi) Koti jeupe lenye mikono mirefu(laboratory coat) kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi tu **(MUHIMU SANA**).

(vii) Suruali nyeusi mbili (2) za kitambaa ambazo mshono ufanane na suruali ya darasani kwa ajili ya kazi za nje baada ya masomo.

**MUHIMU**

**MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUJA NA NGUO YOYOTE YA NYUMBANI TOFAUTI NA SARE ZA SHULE, ANAPOKUJA AJE AMEVAA NGUO MOJAWAPO AMBAYO NI SARE YA SHULE.**

THE HEADMASTER
LUPEMBE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 114
NJOMBE

**BELNOW B MHANGA**

**MKUU WA SHULE**

**2. MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJANAYO SHULENI.**

(i) Ream ya karatasi mbili (2) A4 (kwa mwaka).
(ii) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(orodha imeambatanishwa).
(iii) Dissecting kit kwa wanafunzi wa biology.
(iv) Scientific calculator original.
(v) Godoro la ft.21/ 2 la Dodoma (Ni muhimu sana).
(vi) Mashuka mawili rangi pink, foronya ya rangi ya pink na mtowake blanketi zito moja (1).
(vii) Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko vya bati/mfupa mgumu siyo plastic) pamoja na dumu la lita tano kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa.

**3. VIFAA VYA USAFI NA KAZI ZA NJE.**

(i) Kwa mchepuo wa **CBG** Aje na jembe yenye mpini, ndoo moja ndogo ya lita kumi kwa ajili ya usafi binafsi, ndoo moja ya lita 20 kwa matumizi ya shule, soft bloom moja, mopa(squizer), kwanja (slasher) na fagio ndefu la kutumia buibui.
(ii) Kwa mchepuo wa **EGM** ajena ndoo moja ndogo ya lita kumi kwa ajili ya usafi binafsi, ndoo moja ya lita 20 kwa matumizi ya shule, brush ngumu (hard bloom), mopa (squizer), kwanja (slasher), brush fupi ya tundu la choo yenye mpini mgumu, chelewa kubwa na panga.
(iii) Tochi kwa matumizi binafsi nyakati za usiku ni muhimu sana ingawa umeme upo. Tochi hiyo iwe ya betri au mwanga wa jua **(asije na charger yake).**
(iv) Aje na bima ya afya ya Tsh 50,400 au fedha ili ashughulikiwe shule, cheti cha kuzaliwa na result slip pamoja na folder file moja na box file kwa ajili ya kuhifadhia mitihani yake.
(v) Madaftari makubwa10 (counter bookQ3) au zaidi,pen,penseli,rula na mkebe.

**4. VIFAA VYA USAFI BINAFSI.**

(i) Toilet paper zakutosha muhula mzima walau zianzie tano.
(ii) Taulo la kuogea moja.
(iii) Medicated soap (sabuni za kuogea zenye dawa) ziwe tano (5), miswaki minne (4) ,dawa ya meno, kiwi, brush ya kuogea, ndala na dodoki la kuogea.

**NB VIFAA VYOTE BINAFSI VIWEKEWE ALAMA YA KUDUMUTANIBIHI: Kwa anayetaka kununua shuleni, vitu vifuatavyo vinapatikana katika mazingira jirani na shule.**

- **Vifaa vya Binafsi**

**(Tai, sweta, nguo za michezo, mashati meupe ya shule, soksi nyeusi, soksi bluu(michezo), raba za michezo, truck suti zote, pullneck mashuka, tshirt form six maili,taulo,mto na foronya, godoro(dodoma), na vifaa vya usafi binafsi vyote)**

- **Vifaa vya usafi wa mazingira**

**jembe , panga, ndoo zote, soft bloom, hard bloom, kwanja, chelewa, na brush fupi ya chooni,fagio ndefu ya kutolea buibui,**

THE HEADMASTER
LUPEMBE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 114
NJOMBE

**BELNOW B MHANGA**

**MKUU WA SHULE**

## 5. MICHANGO MBALIMBALI

Michango yote italipwa kupitia akaunti namba **60601000014 NMB BANK** Jina la akaunti **LUPEMBE SECONDARY SCHOOL REVENUE COLLECTI.**

Tafadhari andika jina la mwanafunzi na mchepuo wake kwenye pay in slip. Pindi afikapo shuleni aiwasilishe hati ya malipo kwa mhasibu wa shule.

Mchanganuo wa michango ya Shule upo kwenye jedwalihapo chini.

| **Na** | **Aina ya Mchango** | **Kiasi** |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **JUMLA** | **80,000/=** |

## 6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu naOfisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na.

### (a) Sheria na Kanuni za Shule

(i) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenginenajamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(ii) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.

(iii) Kushiriki kwa kikamili fuma somo ya usiku(Preparation).

(iv) Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa.

(v) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(vi) Kutunza usafi wamwili, mavazi na mazingira ya shule.

(vii) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

(viii) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

(ix) Kutunza mali za shule.

(x) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

1. **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi (MWANAFUNZI YEYOTE ATAKAYEKUTWA NA SIMU SHULENI ATAFUKUZWA SHULE)..**

2. **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu.**

3. **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

## (b) Makosa yatakayo sababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shuleni pamo jana

(i) Wizi.

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyoteyule.

(vi) Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwana nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi

wa shule.

(vii) Kufugandevu.

(viii) Uleviauunywaji wapombe namatumizi ya dawaza kulevya.

(ix) Uvutaji wa sigara.

(x) Uasherati,mahusiano ya jinsimoja, kuoa au kuolewa.

(xi) Kusababisha mimba.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xiii) Kwenda kwenye nyumba zastarehe na nyumbaza kulala wageni.

(xiv) Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xv) Kudharau Bendera ya Taifa.

(xvi) Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

(xvii) Uharibifuwa mali ya umma kwa makusudi.

## 6. VIAMBATISHONAFOMU MUHIMU

(i) Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali.

(ii) Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkatabawa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

(iii) Fomu ya mzazi kukiri kukubalianana sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.

(iv) Picha nne(4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**N.B Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

THE HEADMASTER
LUPEMBE SEC. SCHOOL
P.O.BOX 114
NJOMBE

**BELNOW B MHANGA**
**MKUU WA SHULE**

**7. MAELEZO BINAFSIYAHUSUYOMWANAFUNZI:**

(a) (i) Jina la mwanafunzi…………………...........…………....…………….

(ii) Tarehe ya kuzaliwa…………………………………...………………

(iii) Mahali alipozaliwa(wilaya)……..............………. (mkoa)……………

(iv) Dini………………………..Dhehebu………....……….……………….

(b) Jina la mzazi/mlezi anayekutunza…....................................................
Kazi ya mzazi/mlezi..........................................................................…
Anwani ya mzazi/mlezi.......................................namba ya simu………..……

Mahali anapoishi mzazi/mlezi mkoa……………wilaya……..................…….
Kijiji/mji…………………………………kata…..............................................

(c) Jinala anayekulipia michango ya shule………….........................................

uhusiano……………………..................Anwani yake…........................Namba ya simu……………………………..

(d) Anwani za ofisi ya katibu kata au mwenyekiti wa mtaa/kijiji ambako mzazi/mlezi wa mwanafunzi anaishi: .Jina la kata…………………………..
Anwani…………………………….Nambaya simu......................................…
Jina la mwenyekiti wa kijiji/mtaa..................................................................…
Kijiji/mtaa…………………………………………………….……
Anwani………………………………………Namba ya simu.......................

(e) Jina la ndugu wa karibu…………………………......... .Kijiji/mtaa wa …………………Anwani…………………Namba za simu…..............………

## 8. FOMU YA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.

**MWANAFUNZI:** Mimi…………………………………………….kidato ………….. Nakubali kujiunga na shule hii ya sekondari Lupembe nikiwa mwanafunzi wa Bweni. Nimesoma na kuyaelewa maelezo yote, sheria na taratibu zote za shule. Ninakubali kuingia kidato cha tano katika shule ya sekondari Lupembe. Kwa hiyo ninaahidi kwamba

1. Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu.
2. Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vile ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa chama tawala na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.
3. Nitatunza mali ya uma ambayo ni pamoja na mazingira, samani, vitabu nk.
4. Nitasoma kwa bidii na juhudi ili nifaulu.
5. Nitashiriki katika shughuli nyingine za nje mbali na masomo ya darasani. Sahihi ya mwanafunzi………………………. tarehe………………………

**MZAZI/MLEZI**: Mimi...............................................................ninakubali mtoto wangu .................................. kujiunga shule ya sekondari Lupembe kidato…………mwaka/20 tarehe…................ ............................................................akiwa mwanafunzi wabweni. Kwahiyo naahidi kwamba:- 1.Nitashirikiana kikamilifu na uongozi wa shule, walimu na wafanyakazi wengine wa shule katika kumuelimisha na kumlea mtoto wangu. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa anazingatia sheria, kanuni na taratibu zote za shule na kuyatimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa hapo juu. 2. Nitafanya kila niwezalo ili kumwezesha mwanangu kufika shuleni mapema, kuwa na mazingira mazuri ya kujifunza na kufaulukwa muda wote awapo shuleni.

Anwani yangu ya kudumuni…………………………………………………………

Namba ya simu ya mzazi/mlezi…………………. Email…………………………………

Sahihi ya mzazi/mlezi……………..……tarehe…………………….

# FORM FOR MEDICAL EXAMINATION
# LUPEMBE SECONDARY SCHOOL
# P. O. BOX 114 NJOMBE

**DATE:… ................................ THE MEDICAL OFFICER………………………………**

To be completed by a medical officer in respect of all form five students

1. Name.........................................................................................................................
2. Age …………..………..........years................................................ Sex.......................
3. Blood count(red and white)…………………………………………........………...
4. Stool examination……………………………………………………………..…
5. Urine analysis………………………………………………………………………
6. Eye test………………………………………………………………………..
7. T.B test………………………………………………..……………......……
8. Ears…………………………………………………………………………………
9. Chest………………………………………………………………………………
10. Spleen………………………………………………………...……….........
11. Abdomen……………………………………………………..…………………
12. ADDITIONAL INFORMATION eg. Physical defects or important infections, chronic of family diseases etc.........................................................................................

..............................................................................................................................

SIGNATURE……………………………

DATE……………..…..........................



THE HEADMASTER
LUPEMBE SEC. SCHOOL
P. O. BOX 114
NJOMBE

**BELNOW B MHANGA**
**MKUU WA SHULE**

**ORODHA YA BAADHI YA VITABU KWA KILASOMO**

A. CHEMISTRY

- Advanced chemistry Review by Willam W Davis(Mzumbe bookshop project 2004)
- Physical chemistry by Delungu et(Mzumbe bookshop project 1998)
- Advanced level in organic chemistry part I and II(TIE 1995)
- Organic chemistry volume I.The fundamental principles by I.L Finar(Longman Ltd 1990)
- Ngaiza's Series Of Advanced Chemistry Physical Chemistry 2014.
- Ngaiza's Series Of Advanced Chemistry Organic Chemistry 2014
- Ngaiza's Series Of Advanced Chemistry Inorganic Chemistry 2014

B. BIOLOGY

- New understanding Biology by Suzan Tool
- Advanced biology by Michael Kent
- Biological science third by D.J.Tylor, N.P.O Green and G.W.Stout
- Advanced biology principle and applicationby C.J.Clegg and D.G.McKean
- New understanding biology for advanced level by Glenn and Suzan Tool Plant and animal biology vol.1•&2 by A.E. Vines and N.Rees
- Biology for class XI&XII by Dr.P.S.Verma and Dr. B.P.Pandey
- Biological science by CHANDS Biology by Msaki series (classification, genetics and cytology)

C. GEOGRAPHY

- Principle of physical geography by F.J.Monkhouse
- Geography Integrated Approach by D.Waugh
- Practical geography for Africa by J.M.Pritchard
- General geography in diagram by R.B.Bunnert
- Essentials of Practical Geography by Josephat Mwita
- Simplified physical geography(A level) by D.M
- Statistical methods and the geographers
- Human and Economic Geography by Morgan goh cheng leon

D. ADVANCED MATHEMATICS.

- Chandi I& Ii
- Backhouse I& I
- Pure Mathematics I & II
- Understanding Advanced Mathematics
- Engeneering Mathematics Pure Mathematics (Tranter)

- Reviews Advanced Mathematics 1 & 2 Kinunda
- Understanding Mathematics

E. BASIC APPLIED MATHEMATICS

- Basic Applied Mathematics by Kiza and Septine I.Sillem
- Basic Applied Mathematics by TIE Pure mathematics I•&II by Bank house Core
- course Mathematics by Biotech and Chandler

F. ECONOMICS

- MORDEN ECONOMIC ROBERT MUDIDA
- ECONOMICS 1 ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
- ECONOMICS 1I ACTIVE - ZISTI KAMILI 2010 SYLLABUS
- ECONOMICS A/LEVEL PAPER 1 AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILE NEW SYLABUS
- ECONOMIC A/LEVEL PAPER 1I AND PROFESSIONAL STUDIES – C.M.AMBIKILENEW SYLABUS
- ESSENTIALS FOR A LEVEL ECONOMICS PAPER 1 FORM 5&6 BY AMBROSS ODHIAMBO
- ESSENTIALS FOR A LEVEL ECONOMICS PAPER 1 FORM 5&6 BY AMBROSS ODHIAMBO F.

G. GENERAL STUDIES

- General studies for A-Level certificate form v
- Contemporary approach for A-level general studies
- Notes for form five and six General studies supplementary book for A level and colleges
- Advanced level general studies notes for form 5 and 6 by Nyambari Nyangwine 2009
- General studies for A-Level certificate form v and vi by Richard R.F.

**NB MWANAFUNZI LAZIMA AWE NA KITABU KIMOJAWAPO KWA KILA SOMO LA TAHASUSI YAKE. SIMU HAZIRUHUSIWI KABISA SHULENI**

**NB:Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI /MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA. NAMBA ZA KUTUMIA FEDHA KWA MAHITAJI YA MWANAFUNZI NI 0748580772 M-PESA Jina litakalotokea LUPEMBE SCHOOL**

**NB:** **Shule haitashughulikia kesi ya fedha ambayo itakuwa imetumwa na namba tofauti na namba tajwa hapo juu**

**KARIBU SANA LUPEMBE SEKONDARI**

THE HEADMASTER
LUPEMBE SEC. SCHOOL
P.O. BOX 114
NJOMBE

**BELNOW B MHANGA**

**MKUU WA SHULE**